

# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM



## TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI UFADHILI WA MASOMO YA M.A. KISWAHILI (MARUDIO)

**Taasisi ya Taaluma za Kiswahili** ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kwa kushirikiana na **Kampuni ya ALAF Limited** inapenda kutangaza ufadhili wa ada kwa wanafunzi **watatu (3)** waliochaguliwa kusoma **Programu ya M.A. Kiswahili** katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa Mwaka wa Masomo 2022/2023.

### **Mwombaji awe na sifa zifuatazo:**

1. Awe raia wa Tanzania,
2. Awe mhitimu wa BA Kiswahili au programu husiani na kufaulu vizuri katika masomo ya Kiswahili. Kipaumbele kitatolewa kwa wahitimu wa BA (Kiswahili),
3. Awe na WAKIA (GPA) usiopungua 3.8 wa Digrii ya Kwanza,
4. Awe amepata udahili katika Programu ya MA (Kiswahili) ya UDSM,
5. Awe na umri usiozidi miaka 35 wakati analeta maombi,
6. Awe mhitaji wa ufadhili wa ada,
7. Awe na uwezo wa kujigharimia mahitaji mengine (chakula, steshenari, malazi, utafiti n.k.).

### **Nyaraka Muhimu za Kutuma:**

1. Barua ya maombi ambayo pia itabainisha uwezo wa kitaaluma,
2. Nakala ya cheti cha matokeo ya kitaaluma ya Shahada ya Kwanza (Transcript),
3. Nakala ya cheti cha kuzaliwa,
4. Maelezo mafupi (ukurasa mmoja) yanayobainisha sababu za kuhitaji ufadhili wa ada.

### **Maombi yatumwe kwa:**

Mkurugenzi,  
Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

**Baruapepe:** [iks@udsm.ac.tz](mailto:iks@udsm.ac.tz)

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20/11/2022**

---